Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyofanyiwa marekebisho ya mara kwa mara) na Sheria za Ardhi zinatambua usawa na haki za mwanamke.

Ingawa matukio ya unyanyasaji wa mwanamke yamekuwa yakiendelea kila kukicha. Moja ya sababu ambazo zinachangia kuendelea kuwepo kwa matukio hayo ni uelewa mdogo wa jamii juu ya haki za mwanamke katika ardhi.

Kwa mujibu wa sheria za ardhi za mwaka 1999, ardhi yote Tanzania ni mali ya umma na iko chini ya usimamizi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kama mdhamini kwa niaba ya wananchi wote.

Kabla ya kutungwa kwa sheria za ardhi mwaka 1999, sheria iliyotumika ilikuwa ni Sheria ya Ardhi namba 3 ya mwaka 1923.

Sheria hii ilitungwa wakati wa ukoloni na kutumika hadi Mei 2001, ambapo sheria mpya zilizotungwa mwaka 1999 zilipoanza kutumika. Hii sheria haikutambua na kulinda haki za mwanamke katika ardhi.

Bado hadi sasa kuna baadhi ya wanawake wanakabiliwa na changamoto ya kushindwa kumiliki ardhi hali inayochangia umaskini na kundi hilo kushindwa kujikwama kiuchumi.

Baadhi ya wanawake Kata ya Kisaki na Mngazi Halmashauri ya Morogoro wanasema sababu zinazofanya kushindwa kumiliki ardhi ni ukosefu wa elimu, kutojua sheria za ardhi, hivyo kushindwa kuwa na maendeleo na kuwa tegemezi ndani ya jamii.

Leah Patrick anasema, aliachika na kuachiwa watoto, hivyo alilazimika kutafuta haki yake baada ya mumewe kuuza ardhi pasipo kumpatia sehemu yake na watoto.

Anasema kuwa alisimama kidete na kupambania haki kwa kupambana na wazee wa kimila

Mila, desturi kikwazo mwanamke kumiliki ardhi



Moja ya darasa kati ya madarasa yaliyoanzishwa na waangalizi wa haki za ardhi.

na hatimaye akafanikiwa kupata haki yake.

Mwangalizi wa Masuala ya Ardhi Kijiji cha Gomero, Kata ya Kisaki, Tatu Maleta anasema kuwa bado elimu inahitajika zaidi kuwawezesha wanawake wengi kuzijua haki zao, hivyo kumiliki ardhi.

Anasema amekuwa akiwashirikisha wanawake, vijana na wanaume kuhusiana na haki ya masuala ya ardhi ambapo kumekuwa na muitikio mkubwa miongoni mwa makundi hayo jambo linaloleta faraja kwao.

"Bado elimu inahitajika ili kuyafikia makundi mengi kwa kuwa hivi sasa wanawake wengi wanatambua haki zao na hata baadhi ya wanaume wameamka na kuanza kuandika wosia pasipo kuhofu jambo lolote," anasema Maleta.

Anasema kuwa awali wengi walikuwa wakihofo kuandika wosia kwa kuona kama ni jambo la 'uchuro' na kujitabirika kifo, lakini baada ya elimu baadhi yao wameamka na kuwa tayari kuandika wosia ili kuepusha migogoro inayojitokeza pindi kinapotokea kifo.

Maleta anasema kuwa

hata baadhi ya wajane baada ya kupata elimu wamefungua mirathi na kupata haki wanazostahili.

Anasema kuwa awali mfumo dume uliokuwa umejikita katika kijiji hicho ulisababisha wanawake wengi kupoteza haki za kumiliki ardhi ambapo ulianza ngazi ya familia.

"Kwa sasa tumeamka, elimu tunayopewa na mashirika mbalimbali imesaidia wengi kupata haki ya kumiliki ardhi. Mimi kama muangalizi wa masuala ya ardhi nimekuwa nikitoa elimu katika vikundi mbalimbali vya kijamii," anasema.

Anasema kuwa kutokana na kupata hatimiliki za kimila kupitia mkutano mkuu wa kijiji, imesaidia wanaume kutambua kuwa wanawake wana uwezo mkubwa katika masuala mbalimbali.

"Elimu tuliyopata imetuwzesha hata kupata mikopo inayotolewa na halmashauri na kuendesha maisha yetu na kujiongeza kipato," anasema.

Anasema ili kumuinua mwanamke kiuchumi, lazima apate elimu ya kujitambua, kutambua fursa mbalimbali zinazomzunguka pamoja

kijinsia, wengi wanakuwa na uwoga kumiliki mali kwa kuhofia kuibiwa mali zao, kunyang'anywa na wanaume.

"Bado tunanyanyaswa ndani ya jamii, wanawake tunaongoza kufanyiwa vitendo ukatili wa kijinsia, naweza kulima mazao na mume wangu kipindi cha mavuno mwanaume anauza mazao yote na nikimuuliza ugomvi unaanza," anasema Eutropia.

Mratibu wa Dawati la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Daniel Mallya anawataka wanawake kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao kujiendeleza na kuepuka kuwa tegemezi, na kuwataka kwa mujibu wa sheria ya ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 mwanamke anapaswa kumiliki ardhi.

Mallya anasema inawasapa wanawake kujituma katika uzalishaji, kutumia elimu wanayopewa na wadau mbalimbali katika kuelimisha wanawake wengine ndani ya familia ili kuepuka kuwa tegemezi.

Moja ya kampeni iliyowahi kuzinduliwa nchini inayojulikana kama kampeni ya 'Linda ardhi ya mwanamke' iliyoratibiwa na asasi za kiraia 26, inasema wanawake nchini wanashindwa kumiliki ardhi kutokana na mila na desturi kandamizi ambazo zinaonekana kuwa kikwazo kwao.

Mwenyekiti wa kampeni hiyo, Tike Mwambipile anasema, lengo la kampeni hiyo ni kufunga ombwe lililopo kati ya sera au sheria na taratibu za maisha ya kila siku ya jamii ikiwemo kubadili fikra za watu kutoka mila kandamizi zinazozuia mwanamke kumiliki ardhi.

MABIBO GETWELL DRIVING SCHOOL

- MABINGWA WA KUFUNDISHA UDEREVA MAHIRI.
- MAFUNZO NI MWEZI MMOJA.
- CHUO KINA WAKUFUNZI WENYE UZOEFU MKUBWA.
- HUDUMA YA HOSTELI IPO KWA BEI NAFUU KWA WANAOTOKA NJE YA DAR ES -SALAAM.



CHUO KIPO MABIBO TUNATAZAMANA NA CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI (NIT).

MAWASILIANO:- +255 754 391 536,
+255 656 805 257.

JUKWAA LA UCHUMI



Jiji la Mbeja lilivyojipanga kudhibiti ujengaji holela

UK.12+13



MDAU wa Shirika la Maendeleo la Jamii la Wafugaji wa Asili Tanzania (PAICODEO) Monica Kurumbe akitoa elimu kwa wanawake wa jamii ya wafugaji wilayani Mvomero.



BAADHI ya wananchi wa Kijiji cha Masisiwe wilayani Kilolo Mkoa wa Iringa wakipewa elimu ya ulimiki wa ardhi na Ofisa wa Hakiardhi Kumbuka Mwakyusa.

Ukatili kijinsia unavyoathiri umiliki mali kwa wanawake

NA MWANDISHI WETU

CHANGAMOTO za vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, zimeendelea kuwa kikwazo kwa wanawake hususan kumiliki mali ikiwemo ardhi.

Ukatili huo umechangia baadhi ya wanawake kushindwa kuzungumzia haki zao mbele ya wanaume, na hivyo kuendelea kubaki nyuma kwenye nyanja ya uchumi.

Maeneo yenye viwango vya juu vya ukatili wa kijinsia, wanawake hawana uhuru wa kutoa maoni, kuanzia ngazi ya familia hadi kwenye jamii, jambo linalochangiwa na ukandamizaji unaofanywa na baadhi ya wanaume.

Changamoto hiyo inajitokeza zaidi kwa wanawake katika familia ya wafugaji, ambao licha ya kufanyiwa ukatili na wanaume bado hawako tayari kutoa taarifa kwa vyombo vya sheria.

Joyce Joseph kutoka jamii ya wafugaji wilayani Mvomero mkoani Morogoro, anasema ni kweli wanawake wengi hupigwa na wanaume zao, lakini hukaa kimya kwani hata wakitoa faarifa bado hawapati msaada.

"Ni kweli tunapigwa, hatutakiwi kumiliki mali hususan ardhi na hata tukipigania haki juhudi zetu hugonga mwamba, hivyo ni bora tukae kimya tu, ili maisha mengine yaendelee," anasema Joyce.

Ukatili wa kijinsia kwa wanawake, una taswira na vyanzo vingi kulingana na simulizi za wanawake, kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini, yaliyotembelewa na wadau wa maendeleo ambao wanapigania kundi hilo kumiliki mali.

Kuna vijiji ambavyo kina mama wanaelezea vitu vinavyosababisha mwanamke kupigwa, huku wengine wakisema hakuna sababu yoyote inayohalalisha kupigwa.

Marry Tito mama wa watoto saba, ambaye pia ni mdau wa Haki Ardhi anasema kuna wakati wanatumia muda mwingi kisimani, kutokana na uhaba wa maji unaosababishwa na msimu wa ukame katika kipindi cha kiangazi.

Anasema wanapochelewa kurudi nyumbani wanaume zao huwapiga, kutokana na kutowaamini kuwa walikuwa kisimani muda huo wote, jambo ambalo ni ukatili.

Baadhi ya wanawake wanasema ukatili

wa majumbani unatakiwa kukomeshwa, lakini kutokana na mazingira wanayoishi, hawana namna ya kuepuka vitendo hivyo na hivyo kubaki wanyonge.

Penina Adamu mama wa watoto tisa, anasimulia kwamba kuna wanawake wengine wameshindwa kumiliki ardhi, kutokana na mfumo dume kwa baadhi ya jamii.

"Tutafanyaje? Tunaishia kulia tu na kwenda kulala vyumba vya watoto wetu, kwani hatuwezi kuwaacha watu wetu, hivyo tunalazimika kuendelea kuwepo japo tunakuwa hatuna sauti katika familia zetu," anaeleza Penia.



Tutafanyaje? Tunaishia kulia tu na kwenda kulala vyumba vya watoto wetu, kwani hatuwezi kuwaacha watoto wetu...

Penia Adam Mkazi wa Mvomero

Anasema baadhi ya wanaume kijijini kwao wanapiga wanawake mahali popote, bila uwoga na wakati mwingine hata ukiwa mjamzito wao hawajali, kazi ni kupiga tu na hata kukufukuza nyumbani.

Mary Fadaina mama wa watoto wanane, anasema mwanamke akiama kutoa taarifa, utetezi wake hutegemea nani mwenyekiti wa kijiji, kwani kama kiongozi ni wa jamii yao hakuna hatua zinazochukuliwa.

"Kama Mwenyekiti atakuwa ni wa jamii ya wafugaji, basi hakuna lolote linaloendelea, kwani hata yeye huenda anamfanyia mkewe ukatili, lakini kama mwenyekiti siyo wa jamii yetu hapo tunapata msaada," anasema Mary.

Ukatili wa kijinsia hutumiwa na wanaume kuwakandamiza wanawake

washirikiki katika kuamua, ikiwamo kushindwa kumiliki ardhi, hivyo hubaki kwa wanaume pekee.

Patrida Tengayo anasimulia "Nilikuwa nikikodisha ardhi, nikilima, kuuza mazao na kufanya shughuli zangu zote za napata fedha, mume wangu alikuwa ananipiga akitaka nimpe fedha zote nilizozipata.

"Fedha alizitumia kununua pombe na kufanya matumizi mengine ya anasa nje ya familia, anaporudi nyumbani akiwa amelewa hunipiga. Hakuna nilichofanya kwani katika mila za kimasai hakuna kitu kinachoitwa talaka."

Patrida anaeleza kwamba badaye alijanjaruka na kuficha baadhi ya fedha, ambapo hakutaka kumwambia mipango yake, bado aliendelea kupigwa.

"Nina watoto wanne ambao wananitegemea, hivyo inabidi nijifunze namna ya kutafuta maisha, kwani sijui vipigo vitaisha lini lakini kwa sasa nina ujasiri wa kuficha fedha," anasema.

Lusia Kagangina anasema katika Kijiji cha Wami Dakawa wilayani Mvomero, hakuna tofauti kwani mume akikupiga na ukakimbilia kwa wazazi, utapokea kipigo kingine kutoka kwa wazazi au ndugu wengine.

Mwanaume huo mke mwingine, bila kumshirikisha mkewe, jukumu la mke akisikia mume analeta mwanamke mwingine, anatakiwa aombe marafiki waje kumsaidia, kuandaa chakula cha bila kuhoji kitu.

John Mabula mkazi wa Mkundi Manispaa ya Morogoro anaema kuwa jamii nyingi hasa wa upande wa wanaume kutokuwa na elimu juu ya haki ardhi, ndiyo sababu ya kuendelea mfumo dume ambapo ameishikuru Taasisi ya Haki Ardhi, ambayo imekuwa ikitoa elimu kuelimisha jamii.

Sera na sheria hii imeeleza kuwa makundi yote nchini ni haki yao kupata na kutumia ikiwa ni pamoja na kunufaika na rasilimali mbalimbali, kama ardhi hususan kundi la wanawake ambao ndiyo tegemeo kuwa nchini.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara 24(1) inaeleza kuwa kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, kuwa na haki ya kuhifadhi mali yake kwa mujibu wa sheria zilizo hapa nchini.

Kutokana na ibara hii ya katiba, ni wazi

kuwa wanawake wana haki sawa ya kumiliki ardhi kisheria kama wanaume.

Baadhi ya jamii hapa nchini, zimekuwa zikibagua wanawake katika umiliki ardhi, ikiwemo kutomshirikisha kwenye mambo mbalimbali ya kupitisha uamuzi kuhusu maombi ya hati miliki hususan za kimila.

Ili kuhakikisha changamoto ya wanawake kunyimwa fursa ya kumiliki ardhi, kutomshirikisha kwenye maamuzi yanayohusu ardhi Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), imeamua kumkomboa mwanamke.

Taasisi hii imeamua kumkomboa mwanamke katika jamii kwa kutoa elimu ya kisheria juu ya haki za ardhi, maeneo mbalimbali nchini kwa lengo kuelimisha jamii hasa wanawake mambo muhimu yanayohusu umiliki wa ardhi.

Joseph Chiombola ni Ofisa Program Mwandamizi wa Hakiardhi anasema taasisi hiyo, imeamua kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo ili kutoa fursa kwa wananchi, hususan wanawake kutambua haki ya kumiliki ardhi.

Chiombola anasema lengo kuu ni kukuza uelewa kwa jamii juu ya mfumo wa kumiliki ardhi, ikiwemo kutumia kisheria ili wananchi waweze kutetea, kulinda na kudai haki zao kama vile rasilimali ya ardhi kwa ufanisi.

Chiombola ambaye kitaaluma ni Mwanasheria anasema katika Tanzania imegawanyika katika makundi matatu, ambayo ni ardhi ya kijiji, hifadhi na jumla, ambapo anafanua kuwa ardhi ya kijiji ni ile iliyo ndani ya mipaka ya kijiji.

Ardhi ya hifadhi ni ile iliyotengwa kwa ajili ya matumizi maalumu, kama hifadhi za taifa za wanayapori, milima, misitu na barabara. Ardhi ya jumla ni ile iliyobaki baada ya kuondoa kijiji na hifadhi kwa mujibu wa sheria za nchi.

Anaeleza mujibu wa sheria za katiba ya nchi hii, kifungu cha 3(2) za sheria za ardhi namba tatu na tano kinaainisha kuwa mwanamke ana haki ya kupata, kumiliki, kutumia, kuigawa au kuuza kama vile mwanaume alivyo na haki hiyo.

Chiombola anasema kutokana na changamoto kutoka kwa baadhi ya wananchi, hususan wanawake kutojua sheria za haki ya ardhi taasisi hiyo inatoa elimu ya haki hiyo, ili jamii ielimike na kuepuka migogoro.

"Baada ya kufanya utafiti wa kina imebainika kuwa baadhi ya watu hususan wanawake hudhulumiwa ardhi yao, kwa kutojua haki za ardhi kitendo ambacho kimekuwa kikichochea migogoro ya ardhi nchini," anasema Chiombola.

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto umeendelea kupigwa vita kila kona ya nchi, serikali imeendelea kushirikiana na wadau kuelimisha jamii na kuhakikisha viongozi kuanzia ngazi ya serikali za mitaa na vijiji wanachukua hatua dhidi ya vitendo hivyo.

Mgogoro wa wanakijiji na hifadhi waweka rehani maendeleo ya kilimo

NA WARIOBA IGOMBE

KAMWE huwezi kuliona chozi la samaki hata anapokuwa anapambana kujinasua kwenye nyavu za mvuvi. Machozi yake yote huishia baharini, ziwani au mtoni bila binadamu kuyashuhudia.

Mfano huu hauna tofauti na maswahibu waliyoyapata wakulima wa vitongoji viwili vya shamba la Saba na Mpande kutoka Kijiji cha Ijia, Tarafa ya Mngeta, Halmashauri ya Mlimba wilayani Kilombero mkoani Morogoro.

Wakulima hao wapatao 800 wametakiwa kuondoka katika maeneo yao ambayo wamekuwa wakiyatumia kwa kilimo cha mpunga.

Mkazi wa Kijiji cha Ijia, Kitongoji cha Shamba la Saba, Henrick Jonas, anasema wanapitia kipindi kigumu cha kupoteza mazao na ardhi waliyomiliki kwa muda mrefu.

Anasema muda mrefu wamekuwa wakimiliki ardhi hiyo katika vitongoji hivyo kwa shughuli za kilimo cha mpunga kama njia ya kujipatia kipato cha kujikimu kimaisha.

Anasema kuwa kabla ya kijiji hicho kuitwa Ijia kilikuwa kikiitwa Ikolongo kikihusisha vitongoji vya Toa, Lukolongo na Mbasaa ambapo mwaka 2008 Kitongoji cha Ikolongo kiliingia katika mpango wa matumizi bora ya ardhi.

"Alikuwa ofisa ardhi kutoka Ifakara kutoa semina ya matumizi bora ya ardhi, kijiji kilimpokea mimi nikawa miongoni mwa watu 10 wa kamati iliyohusika na urasimishaji wa matumizi bora ya ardhi katika kijiji chetu," anasema.

Anasema kurasimisha matumizi bora ya ardhi katika kijiji hicho kuna sehemu iliingia katika Shamba la saba kisha kuwekwa mipaka, lakini mwaka 2012 wakaibuka watu wengine kuweka upya alama za mipaka.

Kwa mujibu wa mwana

kijiji huyo, watu hao walielezwa wanatoka Mamlaka ya Usimamizi ya Wanyamapori (TAWA) katika Hifadhi ya Pori Tengefu la Kilombero.

Anaeleza kuwa walifika kuweka alama hizo kwa madai wananchi wa kijiji hicho wamevamia eneo la hifadhi.

"Watu hawa walivamia kijiji chetu maana hawakupita kwenye ofisi za kijiji isipokuwa walishuka bondeni kuweka alama jambo ambalo limezaa mgogoro kati yao na wananchi wa Shamba la Saba na Mpande," anaeleza Jonas.

Anasema wananchi walisikitishwa kwa kitendo hicho ambapo waliamua kupeleka malalamiko kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero ambaye alifika katika kijiji hicho akiwa na watalamu kuona kama malalamiko hayo yana tija.

"Mkuu wa wilaya wa wakati huo alipofika kijijini kwetu akiwa na watalamu wake tulimuonesha ramani ya michoro, lakini wataalamu hao hawakuweza kumuonyesha michoro, hivyo akaona wananchi wana uhalai wa kuwepo hapa," anasema.

Anasema mwaka 2014 kijiji hicho ikiwa ni pamoja na vitongoji vyote viliingizwa katika mpango wa matumizi bora ya ardhi ambapo wananchi waliendelea kufanya shughuli mbali mbali za kibinadamu ikiwemo kilimo cha mpunga na ufugaji.

Mkulima huyo anasema wananchi wa kijiji hicho wamekuwa wakijipatika kipato kutokana na uzalishaji wa mazao lakini wanasikitika kuona TAWA imeibuka kudai eneo hilo ni lao.

"Tumekuwa tukipigwa, kukamatwa na kupeleka mahabusu na hata sasa wamesema tuliolima mpunga katika eneo hili hatutavuna, wataokuja kuvuna ni magereza na sio sisi wananchi," anadai.

Mkulima mwingine wa kijiji hicho, Bonaventura Mpole, anadai wakulima wamekuwa wakikutwa katika mashamba yao ambapo

wamekuwa wakipigwa na askari wa TAWA.

Mpole anaeleza kilio chao ni cha muda mrefu na kwamba wamekuwa wakipeleka malalamiko yao kwa viongozi mbalimbali lakini bado wanaendelea kunyanyasika.

"Tumelima mpunga na sasa muda wa mavuno umefika lakini kutokana na changamoto tuliyonayo tunaweza tusivune," anaeleza.

Naye, Anna Nyasi, anaiomba serikali iliingalie suala hilo kwani wananchi wa kijiji hicho hususan wanawake wanateseka kwa kukosa maeneo ya kulima.

"Kilimo ndio kila kwetu. Tunaiomba serikali itusaidie ili tuvune mazao yetu, tupate fedha za kujikimu kimaisha," anaeleza.

Kwa upande wake, Meneja wa Pori la Tengefu la Kilombero, Laurence Mkobi, anasema katika Kijiji cha Ijia, Kitongoji cha Shamba la Saba kipo ndani ya hifadhi ya pori hilo, hivyo wananchi wanatakiwa kuwepo.

"Tumeongea na wananchi wa kijiji hiki hasa wa vitongoji vya Shamba la saba na Mpande kuwataka wasiendeleo kufanya shughuli za aina zozote zikiwemo kilimo na ufugaji kwani eneo hili ni hifadhi," anasema Mkobi.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa, anakiri kufahamu tatizo hilo ambapo amewataka wananchi wa Kitongoji cha Shamba la Saba kutoendelea na shughuli zozote kwani suala lao linashughulikiwa.

Anasema kuwa kitendo cha TAWA kuwazuia wananchi ni sahihi na wananchi hawapaswi kukaidi, wanachotakiwa kusubiri maelekezo ya serikali.

"Taarifa niliyonayo ni kuwa wananchi wameingia katika hifadhi, natambua kuna malalamiko mengi kutoka kwa wakulima, lakini hawapaswi kuendeleo na shughuli zao wanaozifanya bali wasubili maelekezo ya serikali," Mlawa, anasema.

Ofisa Programu Mwandamizi wa Hakiardhi, Joseph Chiombola, anasema taasisi yake imeamua kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo nchini ili kutoa fursa kwa wananchi hususan wanawake kutambua masuala ya haki za ardhi.

Chiombola anasema lengo kuu ni kukuza uelewa kwa jamii juu ya mfumo wa kumiliki ardhi ikiwa ni pamoja na kuitumia kisheria ili wananchi waweze kutetea, kulinda na kudai haki zao kama vile rasilimali ya ardhi kwa ufanisi.

Chiombola ambaye kitaaluma ni mwanasheria anasema ardhi ya Tanzania imegawanyika katika makundi matatu ambayo ni ardhi ya kijiji, hifadhi na ardhi ya jumla.

Anafafanua kuwa ardhi ya kijiji ni ile iliyo ndani ya mipaka ya kijiji, ardhi ya hifadhi ni ile iliyotengwa kwa ajili ya matumizi maalum kama vile hifadhi za taifa za wanyamapori, milima, misitu na barabara.

Kadhhalika anasema ardhi ya jumla ni ile iliyobaki baada ya kuondoa kijiji na hifadhi kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Baada ya kufanya utafiti wa kina imebainika kuwa baadhi ya watu hususan wanawake hudhulumiwa ardhi yao kwa kutojua haki za ardhi kitendo ambacho kimekuwa kikichochea migogoro ya ardhi nchini," Chiombola.

Mkulima

Tumekuwa tukipigwa, kukamatwa na kupeleka mahabusu na hata sasa wamesema tuliolima mpunga katika eneo hili hatutavuna, wataokuja kuvuna ni magereza na sio sisi wananchi

Alikuwa ofisa ardhi kutoka Ifakara kutoa semina ya matumizi bora ya ardhi, kijiji kilimpokea mimi nikawa miongoni mwa watu 10 wa kamati iliyohusika na urasimishaji wa matumizi bora ya ardhi katika kijiji chetu.



JUKWAA LA UCHUMI



BEN POL AIBUKA N'ROHO'

STAA wa muziki wa bongo flewa, Benard Paul 'Ben Pol', UK.21

Mke na watoto walivyogeuka mpangaji katika nyumba yao

NA WARIOBA IGOMBE, MOROGORO

BAADHI ya watu hususan wanawake kutojua haki zao za msingi imekuwa changamoto kubwa, inayosababisha kundi hilo kijikuta kwenye wakati mgumu na wengi kuwa na maisha duni ya utegemezi.

Safi Kalamba ni mkazi wa Kijiji cha Dumila wilaya ya Kilosa Mkoa wa Morogoro ni mmoja wa wahanga hao, ambaye amejikuta kwenye wakati mgumu wa kuishi chumba kimoja na familia yake baada ya kudhulumwa.

Mama huyu kwa sasa anaishi chumba moja yeye watoto na mjukuu mmoja, ambapo amewaomba wadau kujitokeza na kumsaidia kupata haki yake ya nyumba, baada ya mumewe kuiuza kwa siri, kisha kutoroka kusikojulikana.

Kilio cha Safi, kimefika kwa mwandishi wa makala hii, ambaye alifika nyumbani kwake, ambapo anasema kutokana kuuzwa kwa nyumba yake, imemlathimu kuishi chumba kimoja yeye na mabinti zake wanne.

"Nina familia ya watoto wanne wote wa kike na mjukuu mmoja, wote tunaishi chumba kimoja tulichosaidiwa na wasamiria wema baada ya nyumba yetu kuuzwa kwa siri na mume wangu na kisha kutoweka nyumbani," anasema Safi.

Anasema mwaka 1995 walifunga ndoa na mume wake Joseph Masalu, ambapo walijaaliwa kupata watoto watano wanne wakiwa wa kike na mmoja wa kiume ambaye alifariki dunia.

Anasimilia kwamba mwaka 2010 walijenga nyumba katika kijiji hicho, ambapo mumewe alikuwa mjenzi wa barabara na mwaka 2015, kwao wilayani Tarime kulitokea na matatizo ya kifamilia, hivyo yeye alienda nyumbani.

"Baada ya kutokea matatizo ya kifamilia huko kwetu Tarime mume wangu aliniruhusu kwenda na akanipa nauli na aliniahidi atanitumia nauli ya kurudi, baada ya wiki mbili jambo ambalo hakulitekeleza," anaeleza Safi.

Baada ya kukaa nyumbani kwao kwa muda mrefu, bila mawasiliano na mumewe wazazi wake walimpa nauli ya kurudi kwake, alipofika alikuta nyumba yake ina watu wengi na alipochunguza aligundua kuwa ni wapangaji.

Safi alieleza kwa wakati huo watoto wake, walikuwa shule za bweni wakisoma, wapangaji walimwambia nyumba hiyo siyo mali yake tena, kwani imeuzwa kwa mtu anayefahamika kwa jina la Juma Katambi.

"Baada ya ukimya wa muda mrefu wa mume wangu, nilirudi kwangu na kukuta nyumba imeuzwa na kisha kupangishwa nililia kwa kitendo hicho, nilipojaribu kumtafuta baba watoto wangu kwa simu sikumpata," anasimulia Safi.

Anasema siku hiyo alilala kwa jirani yake na kulipopambazuka alimtafuta mtu aitwae Juma Katambi, anayedaiwa kuinunua na jibu alilopewa ni kuwa



SAFI Kalamba (anayelia) akiwa na familia yake ya watoto wanne na mjukuu mmoja kwenye chumba kimoja wanachoishi baada ya mumewe kudaiwa kuuzwa nyumba yao, Dumila wilayani Kilosa.

ni kweli nyumba hiyo ameinunua na kwamba taratibu zote za kisheria zimefanyika.

Baada ya majibu hayo, Safi anasema alikwenda polisi kutoa taarifa hiyo, ili aweze kupata msaada ambapo Katambi alitwa na kukubali kununua nyumba hiyo, hivyo kutokana na mama huyo kukosa sehemu ya kuishi alipewa chumba kimoja.

Polisi walimsihi Katambi atumie busara na aweze kumpa chumba kimoja, ili mama huyo apate sehemu ya kijihifidhi na familia yake huku taratibu nyingine za kisheria ikiwemo kumtafuta Masalu aliyeyuza nyumba zikifanyika.

HALI YA MAISHA

Uhuru ilishuhudia Safi na wanawe wakiishi maisha magumu, watotowake ambao ni wanafunzi wa shule za misngi nja sekondari, wanaishi kwa kufanya vibarua.

Aziza Joseph ni mtoto mkubwa wa familia hii, anasema yeye amesoma hadi kidato cha sita na kufaulu vizuri, lakini ameshindwa kutimiza ndoto zake za kuwa mwana sheria kutokana na changamoto zinazowakabili wao.

Juma Katambi anayedaiwa kununua nyumba hiyo, anasema hawezi kuzungumzia suala hilo, endapo Safi anaona ameonewa basi afuatilie anachoona ni sahihi.

Kutokana na hali hiyo mwanamke huyo, amewaboa wadau mbalimbali wakiwemo wa masuala ya kisheria, Haki Ardhi kujitokeza na kumsaidia ili apata haki yake, kwani ana watoto wadogo wanaomtegemea kwa kila kitu.

KAULI YA POLISI

David Mkubwa ni Mkuu wa Kituo

cha Polisi Dumila, mkoani Morogoro, anasema ofisi yake imepokea malalamko hayo na kutoa wito wa Katambi (mnunuzi), kufika haraka katika kituo hicho kwa ajili ya mahojiano.

Mkuba anasema kwa sasa Katambi hayupo kijijini hapo, lakini baada ya kupatikana anatakiwa kufika katika kituo hicho ili hatua za kisheria zianze kufanyika kwa lengo la kutafuta haki kwa kila mtu, hasa mama huyo.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka



Nina familia ya watoto wanne wote wa kike na mjukuu mmoja, wote tunaishi chumba kimoja tulichosaidiwa na wasamiria wema baada ya nyumba yetu kuuzwa kwa siri na mume wangu na kisha kutoweka nyumbani,"

Safi Kalamba, mkazi wa Dumila.

1977 ibara 24(1), kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, kuwa na haki ya kuhifadhi mali yake, kwa mujibu wa sheria zilizipo nchini.

Kutokana na ibara hii ya katiba ni wazi kuwa wanawake wana haki sawa ya

kumiliki ardhi kisheria, kama ilivyo kwa wanaume.

Ili kuhakikisha changamoto ya wanawake kunyimwa fursa ya kumiliki ardhi na kutoshirikishwa kwenye mamuzi yanayohusu ardhi.

Taasisi ya Haki ardhi imeamua kumkomboa mwanamke katika jamii kwa kutoa elimu ya kisheria juu ya haki za ardhi, maeneo mbalimbali nchini kwa lengo kuielimisha jamii hususani mwanamke mambo muhimu yanayohusu umiliki wa ardhi.

Joseph Chiombola ni Ofisa Program Mwandamizi wa Haki ardhi anasema, taasisi hiyo imeamua kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo hapa nchini, ili kutoa fursa kwa wananchi hususani wanawake kutambua masuala ya haki za ardhi.

Chiombola anasema lengo kuu ni kukuza uelewa kwa jamii juu ya mfumo wa kumiliki ardhi, ikiwemo kuitumia kisheria ili wananchi watetee, kulinda na kudai haki zao kama vile rasilimali ya ardhi kwa ufanisi.

Chiombola anaeleza kuwa kutokana na changamoto kutoka kwa baadhi ya wananchi hususani wanawake kutojua sheria za haki ya ardhi taasisi yake imeamua kutoa elimu juu ya haki hiyo ili jamii iweze kuelimika na kuepuka migogoro.

Mtaalamu huyu wa sheria anaeleza haki ya mwanamke kwenye suala la kumiliki ardhi ni pamoja na kumiliki ardhi na kumlinda dhidi ya mtu yeyote anayeweza kuchukua uamuzi kuchukua ardhi yake kwa kutumia mabavu.